# KUPAMBANA NA MAGONJWA YA KUKU

## JINSI YA KUTIBU NA KUCHANJA



RLDC
RURAL LIVELIHOOD DEVELOPMENT COMPANY

intercooperation

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

swisscontact

RURAL LIVELIHOOD DEVELOPMENT COMPANY

# RLDC na Uboreshaji wa Maisha Vijijini

Shirika la Rural Livelihood Development Company (RLDC ni moja ya mafanikio ya ushirikaiano kati ya Tanzania na Uswisi kwenye mchakato wa kupambana na umaskini na kuboresha maisha ya jamii za vijijini. Hii ni taasisi isiyo ya kibiashara ili yoanzishwa mwaka 2005 na mashirika ya Intercooperation na Swisscontact, lengo kuu likiwa kutekeleza Programu ya kuendeleza maisha ya jamii za vijijini (RLDP). Programu hii inasha bihiana na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupambana na Umaskini (MKUKUTA). Dhamira kuu ya RLDC ni Kuendeleza/kuboresha mifu mo ya masoko ili kuwawezesha wazalishaji wa vijijini kutumia
fursa zilipo kuboresha maisha yao.

Kwa sasa, RLDC inatelekeleza awamu ya pili ya mpango wake (2008-2011) na inaweka msukumo zaidi kwenye uendelezaji wa mifumo ya masoko. RLDC inafanya kazi katika mikoa sita ya Kanda ya kati-Dodoma, Singida, Morogoro, Shinyanga, Tabora, na Manyara. Jamii nyingi maskini zinaishi katika ukanda huu wenye sehemu kubwa yenye hali ya mvua chache na nusu jangwa inayostawisha shughuli chache za kiuchumi.

Hata hivyo kuna fursa nyingi sana zinazoweza kutoa ajira na kuboresha ya jamii zake. RLDC inafadhiliwa na Serikali ya Uswisi kupitia shirika la Uswisi la maendeleo (SDC).

Kwa sasa RLDC inawezesha sekta  za pamba, alizeti, maziwa, ufugaji wa kuku wa kienyeji, mpunga na habari kupitia vipindi vya redio kwa ajili ya wazalishaji wa vijijini.

**“RLDC inaboresha mifumo ya masoko ili kuwezesha wazalishaji wa vijijini kuinua maisha yao”**







# KUPAMBANA NA MAGONJWA YA KUKU

RLDC
RURAL LIVELIHOOD DEVELOPMENT COMPANY

intercooperation

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development
and Cooperation SDC

swisscontact

# YALIYOMO

| | |
|---|---|
| Utangulizi | 1 |
| Sehemu ya Kwanza | 6 |
| Nyumba ya kulelea Vifaranga | 6 |
| Vyombo kwenye nyumba ya vifaranga | 7 |
| Sehemu ya Pili | 9 |
| Maandalizi kabla na matunzo baada ya kupokea vifaranga | 9 |
| Maandalizi kabla ya kupokea vifaranga | 9 |
| Matunzo baada ya kupokea vifaranga | 9 |
| Ulishaji wa Vifaranga | 12 |
| Sehemu ya Tatu | 14 |
| Chanjo na tiba ya Magonjwa | 14 |

# Utangulizi

Ufugaji wa kuku ni njia rahisi ya kujipatia kipato na lishe bora kwa kaya nyingi za vijijini. Hii ni kutokana na ukweli kwamba:

- Ufugaji hauhitaji mtaji mkubwa kuuanzisha.
- Ni rahisi kuusimamia.
- Faida inapatikana mapema.
- Mali ghafi nyingi zinazohitajika zinapatikana kwa urahisi katika mazingira ya vijijini.
- Kwa kipindi cha hivi karibuni, uzoefu unaonyesha kuwa soko la kuku wa kienyeji linakua na linaelekea kwenye kutokutosheleza wateja.

Pamoja na kuwepo kwa fursa hii nzuri ya kujikwamua kiuchumi, bado haijatumika kikamilifu. Changamoto kubwa iliyopo ni namna ya kudhibiti na kutibu magonjwa ya kuku. Wafugaji wa kuku wanapokuwa wameanza kuona matokeo mazuri ya shughuli hii wengi urudishwa nyuma na kuvunjwa moyo kuendelea kutokana na hasara zinazotokana na magonjwa.

Tatizo hili limeendelea kwa sababu ya:

- Kushindwa kuyatambua vizuri magongwa.
- Kutofahamu njia za kuyadhibiti kwa chanjo na kwa njia nyinginezo hata za asili.
- Kutofahamu tiba sahihi ya magonjwa hayo.
- Kutofahamu taratibu za ufugaji zinazoweza kupunguza matukio ya magonjwa.

Madhumuni ya kijitabu hiki ni kumpa mfugaji mwongozo aweze kutambua dalili za magonjwa mbali mbali ya kuku kwa kina na jinsi ya kuyakinga na kuyatibu. Hatimaye aweze kuwa msaada kwa wafugaji wengine. Mambo yafuatayo yameelezwa katika mwongozo huu:

- Magonjwa ya kuku yanayotokana na virusi.
- Magonjwa ya kuku yanayotokana na bakteria.
- Magonjwa ya kuku yanayotokana na protozoa.
- Wadudu wasumbufu katika kuku.
- Chanjo muhimu kwa kuku.
- Kanuni muhimu za kudhibiti magonjwa.

# Tiba na chanjo dhidi ya magonjwa ya kuku

Afya ya kuku huweza kuathiriwa na magonjwa ya aina nyingi, wadudu tofauti na lishe duni ambavyo husababisha hasara kwa mfugaji yasipodhibitiwa au kutibiwa mapema. Hasara hizo ni pamoja na gharama za matibabu, kushuka kwa utagaji mayai, kudumaa na hata vifo. Sura hii itazingatia zaidi kueleza magonjwa na wadudu pamoja na athari za lishe duni katika uzalishaji wa kuku wa asili.

**Dalili za kuku Mgonjwa**

Dalili za ujumla za kuku mgonjwa ni kama zifuatazo:-

- Kuzubaa
- Kupoteza hamu ya kula
- Kujitenga na wenzake katika kundi
- Kujikunyata
- Kupunguza au kusimama kutaga

**Kumbuka: Ukiona dalili moja au zaidi ya hizi muone mtaalam wa mifugo aliye karibu.**

# Magonjwa ya kuku

Magonjwa yanayoweza kuathiri kuku ni mengi. Magonjwa hayo yamegawanyika katika makundi tofauti kutegemeana na kisababishi chake. Vyanzo vya magonjwa ni virusi, bakteria, protozoa, minyoo, wadudu wa aina mbali mbali na upungufu wa virutubisho kwenye chakula cha kuku na uchafu.

Maelezo katika sehemu inayofuata yanafafanua magonjwa mbalimbali ya kuku katika mtiririko ufuatao:

Magonjwa yanayosababishwa na **virusi, bakteria, protozoa, minyoo, viroboto chawa, utitiri** nk., **lishe duni** na **uchafu.**

# Magonjwa yanayosababishwa na virusi

Kwa kawaida, magonjwa yanayosababishwa na virusi hayatibiki. Hivyo njia pekee ya kukabiliana nayo ni kwa kuchanja ili kuyadhibiti kabla hayajatokea. Ikitokea kuku wakaugua magonjwa yanayosababishwa na virusi, unachotakiwa kufanyika ni kutibu madhara yanayotokana na ugonjwa wenyewe kama itakavyofafanuliwa katika maelezo yafuatayo:

## Mdondo

Ugonjwa unaosumbua sana wafugaji wa kuku ni  Mdondo na wengine huuita Kideri (new castle disease). Chanzo cha ugonjwa huu ni virusi. Ni ugonjwa unaoathiri kuku wa rika zote na mara nyingi humaliza kuku wengi au wote vijijini.

## Dalili  za Mdondo ni:

- Kuku hukohoa
- Kuhema kwa shida
- Hushusha mbawa
- Kupoteza hamu ya kula, kuzubaa, kusinzia
- Manyoya kuvurugika
- Kuharisha kijani
- Kutokwa ute mdomoni na puani
- Kizunguzungu, shingo kujikunja, kurudi kinyumenyume, kupooza mabawa, kuanguka chali, kupoteza fahamu na hatimaye kufa.
- Kuku wengi kwenye kundi hufa katika kipindi kifupi kwa kufikia asilimia 90 hadi 100.




*Baadhi ya dalili za ugonjwa wa Mdondo*

Uenezaji wa ugonjwa huu ni kwa njia zifuatazo:

- Kinyesi cha kuku anayeumwa kikikanyagwa na miguu, magari, baiskeli na kuwafikia kuku nwengine.
- Kwa njia ya hewa (kuvuta hewa yenye virusi ) au upepo waweza kusafirisha virusi.
- Mabaki ya kuku anayeumwa kama utumbo, manyoya n.k. visipozikwa vitaeneza ugonjwa kwa kuku wazima kula mabaki hayo au wanyama watakaokula mabaki hayo huweza kuyasambaza na kueneza ugonjwa.

## Kudhibiti Mdondo

**Kuchanja**

Kwanza kabisa ni chanjo ya Mdondo.
Zipo aina tofauti za chanjo ya Mdondo. Lakini chanjo iliyo rahisi kutumiwa vijijini inaitwa I-2 Thermostable.  Chanjo hii tofauti na chanjo nyingine nyingi inao uwezo wa  kustahimili joto. Hutolewa kwa njia ya kuku kudondoshewa tone moja la dawa katika jicho moja tu. Hii ni dozi kamili kwa kuku wa umri wowote.

Dawa hii upatikana kwenye maduka ya madawa ya mifugo au ofisi za serikali za mifugo.

**Utaratibu wa kuchanja kwa dawa ya I – 2 Thermostable**

- Mdondo hauna tiba kwa hiyo unakingwa kwa chanjo
  Kuku wachanjwe mara baada ya kutotolewa bila kusubiri mzunguko au ratiba ya chanjo inayofuata katika eneo husika.
- Kuku wachanjwe kila baada ya miezi mitatu bila kukosa. Kama unayo kalenda weka alama kwenye tarehe za kuchanja ili uweze kufanya maandalizi mapema ya upatikanaji wa dawa.
- Kuku wachanjwe angalau mwezi mmoja kabla ya mlipuko wa ugonjwa . Kwa kawaida wafugaji wanafahamu miezi ya mlipuko ya ugonjwa huu katika maeneo yao.
- Angalia sana uchanje kuku ambao hawajaambukizwa. Kuku akiishaugua chanjo haitasaidia bali itaongeza kasi ya ugonjwa.
- Japo chanjo ya I-2 Thermostable, ni muhimu ihifadhiwe sehemu kavu na yenye ubaridi wa kawaida isipate joto, la sivyo itaharibika na haitafaa tena kwa chanjo. Pia unaposafirisha dawa hii tumia chombo amacho hakitaruhusu dawa kupata joto. Vile vile wakati wa kuchanja shughuli hii ifanyie kivulini dawa isipate mionzi ya jua.

**Njia nyingine za kudhibiti Mdondo**

- Banda na vyombo vyote vinavyotumika ndani ya banda.viwe safi wakati wote.
- Tenga kuku wageni kwa muda wa wiki 2 na kuwachanja kabla ya kuwachanganya na kuku wenyeji.
  Choma mizoga inayoweza kuletwa kwenye eneo lako.
- Usiruhusu watu kuingia hovyo kwenye banda, ikibidi kuingia watumie viatu ulivyotenga kuingilia bandani kwako Kutoruhusu watu kuingia kwenye banda ovyo.

**Kudhibiti mdondo usienee kutoka vijiji vingine na ndani ya kundi lako:**

- Katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa huu epuka kununua kuku minadani na kutoka sehemu zenye ugonjwa huu.
- Kuku wako wakiugua Mdondo tenganisha wale waliougua ili wasiwaambukize walio wazima.
- Kumbuka kuku akiishaugua usimchanje bali mtenge na mpatie chakula na maji na sehemu nzuri ya kupumzikia.
- Kuku aliyekufa kwa Mdondo azikwe au achomwe
- Kuku aliyechinjwa baada ya kuugua sehemu zake ambazo hazikutumika kama mifupa, utumbo n.k . vizikwe vyote.
- Kuku wengi wakifa kwa ugonjwa huu usilete kuku wengine katika eneo au banda lako hadi angalau upite mwezi mmoja.

**Magonjwa mengine yanayosababishwa na virusi**

| Ugonjwa | Dalili za ugonjwa | Kinga/ tiba |
|---|---|---|
| Ndui ya kuku (Fowl pox)<br><br> | - Vipele vya mviringo ambavyo huweza kuungana na kusababisha vidonda kwenye upanga, masikio na miguu hususan sehemu zisizo na manyonya.<br>- Utando mweupe mdomoni.<br>- Vifo hutokea kwenye vifaranga. | Hakuna tiba<br>Kinga:<br>- Kuku wachanjwe dhidi ya ugonjwa wakiwa na umri wa miezi 2 au kulingana na maelekezo ya mtengenezaji wa chanjo.<br>- Kuku wakiugua wapewe (multivitamini) vitamin na antiobitic kama OTC 20% kutibu vidonda.<br>- Banda liwe safi wakati wote na hasa kudhibiti unyevu.<br>- Kutenga kuku wagonjwa ili wasiambukize wengine. |
| Gumboro | - Ugonjwa huwapata vifaranga wenye umri kati ya wiki 3 hadi 8.<br>- Huambukiza idadi kubwa ya kuku na kusababisha vifo kwa asilimia 20 hadi 50.<br>- Kuku kuharisha kinyesi cha majimaji,<br>- hushindwa kusimama, hutetemeka na hatimaye kufa | Hakuna tiba<br>Kinga:<br>- Chanja vifaranga wakiwa na umri wa siku na urudie kuchanja baada ya siku 21.<br>- Kutenga kuku wagonjwa ili wasiwambukize wengine.<br>- Kuku wapewe antibiotic na vitamin ili kutibu magonjwa nyemelezi |
| Mafua makali ya ndege (Avian influenza) | - Kupumua kwa shida.<br>- Kukohoa na kupiga chafya.<br>- Sehemu za kikole (kidevu na kishungi)) hubadilika na kuwa na rangi ya zambarau.<br>- Kutokwa na machozi,<br>- Kuku kupinda shingo na kuanza kuzunguka.<br>- Kuvimba kichwa<br>- Kuharisha kinyesi chenye maji maji, rangi ya kijani na baadaye kinyesi cheupe. | - Ukiona dalili hizo toa taarifa kwa Daktari/ Mtalaam wa Mifugo aliye karibu nawe.<br>- Ugonjwa huu hauna tiba. |

**Magonjwa yanayosababishwa na Bakteria**

| Ugonjwa | Dalili za ugonjwa | Kinga/ tiba |
|---|---|---|
| Homa ya matumbo (Fowl typhoid) | - Ugonjwa huu unaweza kurithiwa kupitia kwenye mayai au kuambukizwa kutokana na kuku wagonjwa, kinyesi, kudonoana na mazingira machafu.<br>- Kuku huharisha mharo wa njano vilemba na upanga hupauka kutokana na upungufu wa damu,<br>- Manyoya husimama.<br>- Vifo huweza kufikia asilimia 50.<br>- Kuzubaa, kuvimba viungo vya miguu, kuchechemea,<br>- Hukosa hamu ya kula.<br>- Kuku wanaotaga hupunguza utagaji, hutaga mayai yenye ganda laini.<br>- Kuku wanaopona huendelea kusambaza vimelea vinavyosababisha ugonjwa. | - Kuzika au kuchoma moto mizoga na masalia ya kuku waliokufa kwa ugonjwa huo.<br>- Usafi wa banda na mazingira yake.<br>- Ondoa kuku wenye ugonjwa na usitumie mayai yenye ugonjwa kuangua vifaranga.<br>- Tibu kwa kutumia dawa zinazoshauriwa na wataalamu OTC 20% powder<br>- Vile vile vitunguu swaumu hutibu. Chukua robo kilo ya vitunguu swaumu, toa maganda. Kisha twanga, changanya na maji kiasi cha lita moja, chuja na kuwapa maji yake kwa muda wa juma moja. |
| Mafua ya kuku (infections coryza)<br> | - Kutoa machozi<br>- Kuku huvimba uso na macho, kamasi hutiririka toka puani na mdomoni, hukohoa, huhema kwa shida na kukoroma. Mayai hupungua asilimia 10 hadi 40.<br>- Kushindwa kula<br>- Kudhoofika na hatimaye kufa. | - Kinga: usafi wa Banda na mazingira uzingatiwe<br>- Tiba: ugonjwa unatibika kama hatua za uudhibiti zitakuckuliwa mapema (Dawa za antibiotic hutumika mfano OTC 20% ya unga). |
| Kipindupindu cha kuku (Fowl cholera) | - Kuku huhara mharo wa rangi ya njano.<br>- Husinzia na kulegea, hulala | Kinga: Usafi wa banda, vyombo na mazingira yake. |

| | | |
|---|---|---|
| | kichwa kikining'inia kwenye mabawa.<br>- Manyoya husimama, huhema kwa shida, hushindwa kusimama na hatimaye hufa.<br>- Vifo huweza kufikia asilimia 50. | Tiba: Ugonjwa huweza kutibika kwa dawa aina ya salfa. |
| Mharo mweupe (pullorum bacillary diarrhoea) | - Huathiri zaidi vifaranga (kabla ya umri wa wiki 4).<br>- Vifaranga hujikusanya pamoja na kutetemeka kama waliopatwa na baridi.<br>- Huharisha mharo mweupe hamu ya kula hupungua, manyoya hunywea na hupumua kwa taabu.<br>- Vifo huweza kufikia asilimia 50. | - Kama ilivyo kwenye kipindupindu cha kuku |

**Magonjwa yanayosababishwa na Protozoa**

| Ugonjwa | Dalili za ugonjwa | Kinga/ tiba |
|---|---|---|
| Kuhara damu (coccidiosis)<br> | - Kuzubaa.<br>- Kushusha mabawa kama aliyevaa koti.<br>- Kupoteza hamu ya kula.<br>- Kuharisha kinyesi chenye rangi ya kahawia au kilichochanganyika na damu.<br>- Kuharisha damu.<br>- Manyoya kutimka.<br>- Kupauka kwa upanga na ndevu.<br>- Kudhoofika na hatimaye kufa. | Kinga:<br>- kuepuka unyevunyevu katika matandiko.<br>-Kuwatenga kuku wanao onesha dalili za ugonjwa.<br>-Kinga kwa kutumia cooccidiostat.<br>Tiba: ugonjwa huo unaweza kutibika kama hatua za kuudhibiti zitachukuliwa mapema. |

**Athari zinazosababishwa na wadudu**

| Jina la Mdudu | Chanzo | Dalili | Kudhibiti |
|---|---|---|---|
| Viroboto | Uchafu, hasa vumbi ndani ya banda la kuku. Viroboto hujificha na kuazaliana katika vumbi. | Wadudu weusi huonekana wanamshambulia kuku kwenye kishungi, kichwani, na uso kwa ujumla. | Tunza usafi wa banda. Nyunyizia dawa za kuua wadudu katika banda. Kwa mfano Akheri powder au Servin. |
| Papasi chawa na utitiri | Kama hapo juu | Wadudu wadogo wengi husambaa katika mwili mzima wa kuku hunyonya damu. | Kama hapo juu |

**Athari zinazosababishwa na Minyoo**

| Dalili za Ugonjwa wa Minyoo | Kinga Tiba |
|---|---|
| - Kudumaa.<br>- Kuku anakuwa mwepesi au kupungua uzito.<br>- Kukohoa.<br>- Kukonda<br>- Kupauka sehemu sisizo na manyoya kama upanga, ndevu masikio na macho.<br>- Utagaji wa mayai hupungua au kusimama kabisa.<br>- Kuharisha.<br>- Minyoo inaweza kuonekana kwenye kinyesi. | Tiba: minyoo inaweza kutibika kwa kutumia madawa mbali mbali kama itakavyoshauriwa na mtaalam wa mifugo.<br><br>Kinga: Kusafisha vyombo vya chakula na vya kunywea maji kila siku kwa kutumia maji na sabuni au dawa za kuua wadudu.<br>- Kutenganisha kuku wakubwa na wadogo.<br>- Kubadilisha matandazo kwenye sakafu kila baada ya miezi mitatu.<br>- Kuzingatia usafi wa banda.<br>- Kuwapa dawa ya kuzuia aina nyingi za minyoo kila baada ya miezi mitatu. |

**Athari za upungufu wa virutubisho kwenye chakula**

| Dalili za Ugonjwa wa upungufu wa virutubisho ktk chakula | Kinga Tiba |
|---|---|
| - Kudumaa.<br>- Kupungua uzito,<br>- Kulemaa viungo<br>- Kuvunjika mifupa kwa urahisi<br>- Kutaga mayai yenye ganda laini,<br>- Kutaga mayai machache,<br>- Kutoata manyoya yakutosha.<br>- Kunyonyoka na kujikunja manyoya.<br>- Kujaa kwa tumbo, kifua na ngozi. | Tiba: athari zinazotokana na upungufu wa virutubishi zinaweza kurekebishwa kwa kuwapa kuku virutubishi vilivyopungua katika chakula.<br><br>Kinga: Kuwalisha chakula kilicho na mchanganyiko wenye uwiano sahihi katika wanga, protini, vitamini, madini na maji ya kutosha. |

**Dawa za asili za kutibu Magonjwa tofauti ya kuku**

Zipo dawa tofauti za asili zinazopatikana kirahisi kwenye mazingira ya vijijini ambazo zina uwezo wa kutibu magonjwa ya kuku. Katika sehemu hii ya mwongozo tunaeleza baadhi ya dawa hizo.

**Dawa ya vidonda vinavyotokana na Ndui ya kuku au vidonda vingine vyovyote**
**Dalili ya Ndui**

- Kuku hupata vipele vya mviringo kwenye upanga wake wa kichwani, kwenye masikio, miguuni na kwingineko kusikokuwa na manyoya.

**Mmea unaotumika kutibu unaitwa Shubiri mwitu.**



| Jina la Mmea | Lugha |
|---|---|
| Shubiri mwitu | Kiswahili |
| Mkankiruri | Kinyaturu |
| Itembwe | Kigogo |
| Ibhata | Kinyiha |
| Litembwetembwe | Hehe |
| Koli | Kikaguru/Kinguu |
| Aloe | Kiingereza |
| Aloe vera | Kisayansi |

**Kuandaa**

- Chukua majani ya Shubiri mwitu na kuyachana vipande vidogo vidogo. Vitwange na pumba kidogo na kuvianika.
- Vikiisha kauka vitwange na kuchekecha upate unga laini.
- Hifadhi unga katika chombo kisafi na kikavu.

**Kutumia**

- Safisha vidonda vilivyotokana na ndui au vidonda vyovyote vile na maji safi yaliyo na chumvi kiasi.
- Pakaa unga wa Shubiri mwitu katika vidonda vilivyosafishwa.
- Rudia baada ya siku moja. Tumia hivyo hadi vidonda vikauke.

**Kudhibiti magonjwa mengi mengine ya kuku kwa kutumia Shubiri mwitu ni kama ifuatavyo :**
**Kuandaa**

- Chukua jani moja la Shubiri mwitu lenye ukubwa wa kati.
- Likate katika vipande vidogo vidogo.
- Loweka vipande ulivyokata katika maji kiasi cha lita mbili. Kuku utumia maji haya kunywa yakiwa na vipande hivi vya shubiri mwitu hadi unapobadilisha.

**Kutumia**

Kuku watumie maji haya kwa kunywa siku zote. Hii inafanya kazi ya kuwakinga kuku dhidi ya magonjwa mbalimbali. Badilisha maji hayo kabla hayajaanza kuchacha na kuwatengenezea dawa nyingine. Hakikisha chombo kinasafishwa vizuri kabla ya kuwawekea dawa nyingine.



**Dawa ya kutibu Kuku Kuharisha namna yoyote**
Mmea unaotumiwa ni **Mpapai**

**Kuandaa**
Pata jani moja bichi la Mpapai na uliponde ponde lilainike kiasi. Kisha changanya na maji kiasi cha lita mbili na nusu.

Kutumia (kwa tiba)

- Kuku wapewe maji hayo wanywe,wasipewe maji mengine kwa ajili ya kunywa kwa siku angalau nne au zaidi.
- Inafaa zaidi kila siku kuwaandalia dawa mpya ili dawa isiharibike.

**Kutumia (kwa kinga)**

- Hata kama kuku hawaharishi, wakizoeshwa kunywa maji yenye majani ya mpapai yaliyopondwa angalau mara tatu kwa wiki watakingwa magonjwa mengi.

**Njia nyingine ya kutumia Mpapai:**
**Kuandaa na Kutumia**

- Chukua majani ya Mpapai uyatwange upate kisamvu chake kiasi cha lita 1.
- Changanya kisamvu hicho na pumba lita 2.
- Waweza kuongezea maji kidogo na kuwapatia kuku wanaoumwa watumie chakula hicho hadi wapone.

Kama kuku ni wachache, andaa chakula wanachoweza kumaliza kwa siku moja ili kisibakie na kuharibika kabla hawajakimaliza.

# MAMBO MUHIMU YA KUKUMBUKA UNAPOTOA CHANJO NA TIBA

**CHANJO**

- Chanjo hutolewa kutegemeana na aina ya ugonjwa unaotaka kudhibitiwa.

- Chanjo tofauti hutolewa kwa nyakati ratiba/ tofauti , kipimo, na masharti tofauti ya utunzaji wa dawa ya chanjo.

- Chanjo hutolewa kabla ugonjwa haujatokea kwa sababu chanjo imekusudiwa kukinga wala siyo kutibu.

- Ili Chanjo iweze kufanya kazi vizuri hutolewa kwa kuku wenye afya nzuri.

- Endapo chanjo itatolewa kwa kuku anayeumwa haitafanya kazi vizuri badala, yake itaongezea kasi ya ugonjwa na hata kusababisha kifo.

Hivyo ni muhimu kila mfugaji aweze kutambua dalili za kuku wagonjwa ili asifanye makosa ya kuwachanja, badala yake awatibu kwanza, wakishapona ndipo wapate chanjo.

**Kumbukumbu**

Mfugaji anashauriwa atunze kumbukumbu za chanjo na matibabu ili zimsaidie kujua yafuatayo:

- Muda sahihi wa kuanza chanjo na kurudia chanjo.
- Idadi ya kuku wanaotakiwa kuchanjwa muda wa kuchanja ukifika.
- Kiasi cha dawa kinachohitajika (dozi) kuandaliwa.
- Aina ya chanjo inayohitajika kulingana na magonjwa yanayojitokeza mara kwa mara.

**Kushirikiana**

Udhibiti wa magonjwa kwa njia ya chanjo unahitaji nguvu ya pamoja ili kupata matokeo mazuri. Ni vizuri wafugaji kwenye eneo moja wakishiriki kupanga mkakati na kusimamia utekelezaji wa suala zima la uchanjaji. Umuhimu wa kuchanja kuku kwa wakati mmoja katika eneo ni muhumu ili kudhibiti ugonjwa kwa wakati mmoja. Mfugaji anayeamua kuchanja azingatie ratiba ya chanjo ya ugonjwa husika ili kuweza kupata matokeo mazuri.

**Kumbuka siku zote:**

Magonjwa tofauti yana Chanjo tofauti. Chanjo nyingi ni maalum kwa ugonjwa mmoja.

Kama umewachanja kuku wako ili kuwakinga na Mdondo, haina maana kuwa umewakinga na magonjwa yote.

Hivyo, kila ugonjwa unaotakiwa kudhibitiwa kwa chanjo lazima ifanyike chanjo yake tofauti. Nayo ifanywe kwa kuzingatia wakati uliopendekezwa na wataalam.

**TIBA**

Tiba hufanyika baada ya kuona au kutambua kuwa kuku wana dalili za ugonjwa. Mfugaji awe makini kufuatilia afya ya kuku wake ili kubaini matatizo ya ugonjwa mapema. Hii itamsaidia kufanya matibabu mapema kbla hayajaleta madhara makubwa kwa wale wanaoumwa. Pia itakuwezesha kudhibiti ugonjwa mapema ili usiendelee kuenea kwa kuku wengine.

Zingatia yafuatayo unapotoa tiba:

- Toa dawa sahihi kwa ugonjwa husika kufuatana na maelekezo ya mtengenezaji yakiwemo kiasi, muda wa kutoa na ratiba ya kurudia dawa. Vile vile chunguza ukomo wa kutumia dawa ili utumie dawa yenye nguvu inayohitajika.

- Wakati wa kutibu usitumie dawa chini ya kiwango kilichopendekezwa. Ukifanya hivyo vimelea vya ugonjwa unaotibu vitajijengea usugu kwa dawa hiyo na baada ya muda dawa hiyo haitakuwa na nguvu ya kutibu.

- Dawa nyingine zina madhara kwa binadamu iwapo watakula nyama na mayai kutoka kwa kuku walilotibiwa ndani ya kipindi kilichozuiliwa. Hivyo mfugaji asiuze mazao ya kuku kabla kipindi hicho hakijapita ili kumkinga mlaji wa nyama au mayai.

## HITIMISHO

Kumbuka kinga ni bora kuliko tiba. Kanuni za ujumla ya kudhibiti magonjwa katika ufugaji wa kuku ni kuhakikisha yafuatayo:

- Kutunza usafi wa sehemu wanapokaa. Kama unafuga katika banda hakikisha linakuwa safi bila kuwa na unyevu. Wadudu na vimelea vya magonjwa huzaliana kwa urahisi katika mazingira yenye unyevu.

- Hakikisha kuwa vyombo vya kuwalishia na kuwanyweshea maji vinakuwa visafi.

- Hakikisha hawakutani na kuku ambao tayari ni wagonjwa maana wataambukizwa. Inawezekana kufanya hivi kama unafuga nusu ndani na nusu nje kwenye uzio au ndani ya banda.

  Kama unafuga huria watakuwa kwenye hatari zaidi ya kuambukizwa na kuku wengine.

RURAL LIVELIHOOD
DEVELOPMENT COMPANY

Jengo la NBC
Ghorofa ya Pili, Mtaa wa Nyerere
S.L.P. 2978, Dodoma, Tanzania.
Simu +255 26 2321455, Faksi +255 26 2321457.
Barua pepe: info@rldc.co.tz.
Tovuti: www.rldc.co.tz.